




Tina na Nyota



Deogratias Simba

Iddi Marumba







Tina na baba yake, walikuwa wamekaa nje.
Tina alitazama juu. Aliona nyota zinametameta.
Aliuliza, nyota ziko kama vipepeo baba? Baba
alisema, hapana.



Ni za ajabu, zinametameta na kumulikamulika.
Lo, nazitamani sana. Tina alisema, baba, baba,
ninazitamani nyota. Utaninunulia? Baba
alicheka.






Aaa Tina, nyota haziuzwi zinakaa huko juu
tu. Tina aliuliza, utaenda kunichukulia? Baba
alijibu, subiri kidogo Tina, nitakutafutia.



Aaa! Ijumaa iko karibu na Jumamosi, si eti baba ee! Naam, baba alisema, ni kweli, Ijumaa na Jumamosi ni siku zinazofuatana.




Tina alikaa kimya. Kisha alisema, akiwa
mkubwa atakwenda kuzifuata. Wote
wakacheka na kuingia ndani.





Tina alikuwa anacheza. Mara, alitokea malaika. Malaika alimetameta kama zile nyota. Tina alitabasamu akauliza, na mimi naweza kuwa malaika? Malaika alicheka.





Tina wewe ni mtoto mdadisi, unataka nini?
Tina alisema, ninapenda nyota, zinavutia.
Ninazitamani, zinametameta na ninafurahi
ninapozitazama.





Malaika alisema nitakupa mabawa. Alimgusa mgongoni, mara, Tina alipata mabawa. Tina alifurahi sana alisema, asante. Malaika naye alifurahi, kisha alitoweeka.








Tina alipaza sauti alisema, siwezi kwenda
peke yangu kuchuma nyota. Alisema enyi
nyota nakuja kuwachukua. Nyota zilimsikia,
zilimulikamulika zaidi.



Njiwa alipita, alimsikia Tina akiziïta nyota aka-mwendea. Njiwa alimuuliza unaongea na nyota? Tina akajibu, ndiyo. Natafuta rafiki wa kwenda naye.








Tina na njiwa walianza kupaa. Walipaa,
walipaa juu, juu zaidi. Kwenye mlango wa
mbingu, walimkuta babu mlinzi. Wakamuomba
waingie.





Babu akasema, atakayeweza kulijibu swalii hili
ataingia. Nyota moja ukiongeza nyota nne
unapata nyota ngapi? Unapata nyota tano.
Tina alijibu haraka.






Tina hufanya bidii shulenii. Alipenda masomo hasa ya hisabati na kusoma. Babu alifurahi sana alimwambia. Umepata, kila mmoja akachukue nyota tano.




mama, kaka na rafiki yake Fatuma.



Kumbe, Tina alikuwa kwenye ndoto.
Uso wake ulionyesha tabasamu.
Mkono mmoja alikunja ngumi,
Bila shaka alibeba nyota zile tano.





Tina, alicheka kwa sauti.

Wazazi wake walienda chumbani kwa Tina.

Walimtzama mtoto wao.

Mama alimbusu usoni.



Baada ya juma moja. Baba alinunua mfano wa nyota tano kubwa. Zilikuwa na taa ndogondogo. Usiku zilipowashwa, zilikuwa zinametameta na kutoa mwanga mzuri. Tina alifurahi sana. Aliziweka mbili kwenye chumba chake.

